# Orodha ya Ukweli wa Ustahiki wa Chanjo ya COVID-19

Jimbo la Ohio linapanga kutoa chanjo ya COVID-19 kwa yeyote atakayeamua kuipokea. Kwa kuwa kuna uhaba wa chanjo, wanaopewa kipaumbele cha kupokea chanjo hizo mwanzoni ni makundi mahususi ya watu walio hatarini zaidi, kulingana na umri, kazi, hali ya maisha, au historia ya kiafya. Tazama maelezo yaliyo hapa chini ili kufahamu ikiwa unastahiki kupokea chanjo ya COVID-19 sasa hivi katika jimbo la Ohio.

**Mnamo Machi 29, makundi ya wanaostahiki yataongezeka ili kutoa chanjo kwa mtu yeyote anayeweza kuipokea kwa usalama**. Ili kuratibu miadi utakapostahiki, tembelea Huduma ya Ohio ya Usimamizi wa Chanjo (VMS).

## USTAHIKI KULINGANA NA UMRI

- Watu wa umri wa miaka **50 au zaidi**.
- Watu wenye umri wa miaka **40 au zaidi**, kuanzia mnamo Machi 19.

## USTAHIKI KULINGANA NA MAKAZI

- Wakazi **wa vituo vya kutunzia wakongwe na walemavu**.
- Wakazi wa **vituo vya watu wanaohitaji usaidizi wa kuendesha shughuli za kila siku**.
- Wagonjwa katika **hospitali za jimbo zinazohudumia wagonjwa wa akili**.
- Watu wenye ulemavu wa ukuaji wanaoishi katika **makazi ya watu wenye matatizo changamano ya kiafya, au vituo na makazi ya utunzaji wa wakongwe na walemavu.**
- Watu wenye matatizo ya kiakili, ikijumuisha matatizo ya kutumia dawa za kulevya, wanaoishi katika **makazi ya watu wenye matatizo changamano ya kiafya, au vituo na makazi ya utunzaji wa wakongwe na walemavu.**

- Watu wanaoishi katika **makazi ya wastaafu wa jimbo la Ohio yanayoendeshwa na jimbo**.

## USTAHIKI KULINGANA NA ZINAFANYA

- Watu wenye **ujauzito.**
- Watu wenye **aina ya 1 ya kisukari**.
- Watu wenye **aina ya 2 ya kisukari**.
- Watu wenye ugonjwa wa neva wa **ALS, ambao pia unafahamika kama ugonjwa wa Lou Gehrig.**
- Watu wenye **ugonjwa sugu wa figo**.
- Wagonjwa ambao **wamepandikizwa uboho**, katika huduma ambayo pia hufahamika kama upandikizaji wa seli shina, na wanapokea matibabu sanasana ya saratani au aina fulani za anemia
- Watu wanaougua **saratani,** kuanzia mnamo Machi 19.
- Watu wenye **ugonjwa sugu wa figo (CKD),** kuanzia mnamo Machi 19.
- Watu wenye **ugonjwa sugu wa kuziba mapafu (COPD),** kuanzia mnamo Machi 19.
- Watu wenye **maradhi ya moyo,** kuanzia mnamo Machi 19.
- Watu **wanene kupindukia,** kuanzia mnamo Machi 19.
- Watu wenye hali fulani za kiafya ambazo zimekuwepo tangu kuzaliwa au zilizoibuka mapema utotoni. Hali za kiafya zinazostahiki zilizo katika kategoria hii lakini hazijaorodheshwa hapo juu:
    - **Anemia selimundu.**
    - **Udumavu.**
    - **Cystic fibrosis.**
    - **Msinyao wa misuli**.

- **Mpoozo wa ubongo.**
- **Ugweuti mchomozo.**
- Watu **waliozaliwa na matatizo sugu ya moyo** ambayo yanahitaji matibabu maalum ya mara kwa mara.
- **Phenylketonuria (PKU), Tay-Sachs,** na matatizo mengine **nadra ya metaboli yanayorithiwa.**
- **Ugonjwa wa kifafa** wenye mitukutiko isiyoisha; **majimaji kwenye uwazi wa ubongo, tatizo la mtoto kuwa na kichwa kidogo kuliko kawaida,** na matatizo mengine **sugu ya kinyurolojia.**
- **Milimbiko dalili ya Turner, fragile X, Prader-Willi,** na matatizo mengine **sugu ya kijeni.**
- **Pumu kali** ambayo ilimhitaji mgonjwa kulazwa hospitalini katika mwaka uliopita.
- **Upungufu wa himoglobini kwenye damu kutokana na ukosefu wa protini za alfa na beta.**
- **Upandikizaji wa viungo vya mwili** (wanaopokea pamoja na wanaotoa viungo hivyo).

**USTAHIKI KULINGANA NA KAZI**

- **Wafanyakazi** wa huduma za afya na wafanyakazi ambao wanahusika mara kwa mara katika utunzaji wa wagonjwa wa COVID-19.
- **Wanaotoa huduma za**afya za dharura (EMS).
- **Wafanyakazi** wa vituo vya kutunzia wakongwe na walemavu.
- Wafanyakazi katika **makazi ya watu wanaohitaji usaidizi wa kuendesha shughuli za kila siku**.
- Wafanyakazi katika **hospitali za jimbo zinazohudumia wagonjwa wa akili.**
- Wafanyakazi katika **makazi ya watu wenye matatizo changamano ya kiafya, vituo vya utunzaji wa wakongwe na walemavu, au** makazi ya watu wenye ulemavu wa ukuaji.
- Wafanyakazi katika **makazi ya watu wenye matatizo changamano ya kiafya, au vituo** vya utunzaji wa wakongwe na walemavu, au vituo vya watu wenye matatizo ya kiakili, ikijumuisha matatizo ya kutumia dawa za kulevya.
- Wafanyakazi wa **makazi ya wastaafu wa jimbo la Ohio yanayoendeshwa na jimbo**.
- Wafanyakazi katika **shule za K-12** zinazoendesha masomo ya kuhudhuriwa madarasani.
- Watu wanaotoa **huduma za utunzaji wa watoto** na wanaondelea kutangamana moja kwa moja na watoto waliosajiliwa kupokea huduma hizo.
- Watu wanaotoa **huduma za mazishi**.
- Wafanyakazi wanaohudumu kwa saa kamili za kazi **ambao wanadumisha utekelezaji wa sheria** (angalau saa 20 kila wiki) na wana majukumu ya kutoa huduma za dharura au ni wasimamizi wa moja kwa moja.
  Inajumuisha:
  - Maafisa wa polisi.
  - Manaibu wa maliwali.
  - Maafisa wa polisi wanaoshika doria kwenye Barabara Kuu za Jimbo la Ohio.
  - Maafisa wenye majukumu maalum, kama vile wale wanaotekeleza sheria za Idara ya Rasilimali Asili ya Ohio (ODNR), wapelelezi wa bodi ya famasia, maajenti wa BCI, wapelelezi wa jimbo wa mikasa ya moto, maafisa wa shirikisho wa kulinda usalama katika usafiri, pamoja na maafisa wengine wa kutekeleza sheria wa shirikisho ambao hawawezi kupata chanjo kutoka kwa vyanzo vinavyotolewa na shirikisho.
- Wafanyakazi wanaohudumu katika **idara ya kurekebisha tabia**, ikijumuisha wafanyakazi wanaofuatilia tabia za wahalifu walio chini ya uangalizi na wafanyakazi wanaofuatilia tabia za wafungwa walioachiliwa ambao wanatoa huduma za moja kwa moja kwa mtu mfungwa aliye mtu mzima au mtoto, au kwa mtu anayesimamiwa na korti.
- Wafanyakazi wa sasa hivi wa idara **ya zimamoto inayotambulika katika Ohio**.

*Hati hii ilibuniwa mnamo Machi 16, 2021.*

Kwa maelezo ya ziada, tembelea coronavirus.ohio.gov.

Ili kupata majibu ya maswali yako kuhusu COVID-19, piga simu kupitia 1-833-4-ASK-ODH (1-833-427-5634).

**Afya ya akili yako ni muhimu kama ilivyo afya ya mwili wako. Ikiwa wewe au mpendwa wako anashuhudia wasiwasi unaohusiana na janga la COVID-19, kuna usaidizi unaopatikana saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. Piga simu kwa huduma ya usaidizi unaohusiana na COVID-19 kupitia 1-800-720-9616**.